ELIMU TIBA UTAFITI

# CHUO KIKUU CHA AFYA NA SAYANSI SHIRIKISHI, MUHIMBILI

# HOMA YA DENGUE

## Homa ya Dengue ni nini?

Homa ya Dengue Homa ya dengue ni ugonjwa unaosababishwa na kirusi ambacho kinaenezwa na mbu wa aina ya Aedes

Homa ya dengue inaweza kusababishwa na yeyote kati ya aina nne za kirusi cha dengue yaani: DEN-1, DEN-2, DEN-3, and DEN-4. Unaweza kupata uambukizi wa wa angalau aina mbili kama sio aina zote nne katika nyakati tofauti za maisha, lakini ni mara moja tu kwa kila aina.

## Historia na Takwimu

Ugonjwa huu umejulikana na wataalamu wa afya kwa takribani miaka 200 sasa, Dengue in ugonjwa uliosambaa duniani kote hasa katika nchi za ukanda wa joto kama vile visiwa vya Karibbean, Amerika ya kusini na kati, Afrika, mashariki ya mbali ya Asia na China, India, Mashariki ya kati, na Australia. Takribani asilimia 40 ya watu wote duniani wanaishi katika nchi zenye ugonjwa huu. Takwimu za Shirika la Afya Duniani zinathibitisha kuwa takribani matukio milioni 5 ya Dengue yanatolewa taarifa kila mwaka. Watu wapatao laki 5 hulazwa hospitali kwa kuathirika na Dengue kali. Homa ya Dengue imeshatokea katika nchi zipatazo 34 barani Afrika. Hapa Afrika Dengue ni ugonjwa unaojulikana kwa kiwango kidogo sana. Licha ya kwamba milipuko ya kwanza imetokea tangu mwanzoni wa karne ya 19. Matukio ya Ugonjwa huu yameongezeka Afrika tangu miaka ya 1980, matukio mengi yakitokea nchi za ukanda wa Mashariki mwa Afrika ikiwa ni pamoja na Msumbiji, Somalia, Kenya, Komoro, Djibouti na Tanzania. Ikumbukwe kuwa jina “Dengue” linatokana na neno “Dinga” la kiswahili linalolomaanisha ugonjwa unaotakana na pepo yaani Kudinga pepo. Mabaharia wa Kispanish walipokuja kwenye pwani ya Afrika Mashariki walirudi kwao na kuuita “Dengue”

Aidha, mlipuko wa ugonjwa huu si mpya hapa nchini kwani uligundulika kwa mara ya kwanza mnamo Juni 2010 mkoani Dar es Salaam ambapo idadi ya watu 40 walithibitika kuwa na ugonjwa. Pia, kati ya mwezi Mei hadi Julai 2013,wagonjwa 172 walithibitishwa kuugua ugonjwa huu.

## Uambukizi

Kirusi cha homa ya Dengue kinaambukizwa kutoka mtu mmoja hadi mwingine kwa kuumwa na mbu wa Jamii ya Aedes, na hasa Aedes aegypti. Mbu huyu anaishi katika mazingira ya makazi ya binadamu. Huuma wakati ya mchana ndani ya nyumba au kwenye maeneo yenye vivuli, hususani majira ya asubuhi na jioni kabla jua halijazama. Mbu huyu anazaliana katika maji yaliyotuama hasa kwenye vyombo vya nyumbani, makinga maji ya paa za nyumba, matairi ya gari, ndoo, vikopo, na kadhalika. Kwa bahati mbaya mbu huyu huweza kuzaliana katika vifaa vidogo vidogo ambavyo watu wengi huvidharau. Hivi ni pamoja na makopo ya kuotesha maua, vikombe, vifuu vya nazi, na

kadhalika. Majani mapana yanayohifadhi maji ni mazingira mazuri kwa kuzaliana kwa mbu huyu, hivyo maeneo ya bustani siyo ajabu kuwa mahali pazuri kwa mbu hawa. Ugonjwa huu hauambukizi kwa kumhudumia mgonjwa au kugusa majimaji yanayotoka kwa mgonjwa.

## Dalili

Dalili za ugonjwa huu ni homa, kuumwa kichwa, maumivu ya viungo na uchovu. Dalili hizi huanza kujitokeza kuanzia kati ya siku ya 3 na 14 tangu mtu alipoambukizwa kirusi cha homa ya dengue. Kwa wakati mwingine dalili za ugonjwa huu zinaweza kufanana sana na dalili za malaria, hivyo basi wananchi wanaombwa kuwa wakati wakipata homa kuhakikisha wanapima ili kugundua kama wana vimelea vya malaria ua la ili hatua stahiki zichukuliwe. Kuna aina 3 tofauti za namna ugonjwa huu unavyoweza kujitokeza iwapo mtu aking`atwa na mbu mwenye virusi hivi;

i. Homa ya dengue (Dengue Febrile Illness): Aina hii huambatanana dalili kuu tatu za homa kali ya ghafla, kuumwa kichwa na maumivu ya viungo au uchovu.Aidha, kwa Tanzania mpaka sasa zaidi ya asilimia 90 ya wagonjwa wamejitokeza na dalili hizi.

ii. Dengue ya damu (Dengue Haemorrhagic Fever): Aina hii ya homa ya dengue huambatana na dalili za mgonjwa kutokwa na damu kwenye fizi au puani, vile vile kutokwa na damu chini ya ngozi.Iwapo mgonjwa huyu ataumia sehemu yoyote ni rahisi kwake kupoteza damu nyingi kupitia kwenye michubuko.

iii. Dengue ya kupoteza fahamu (Dengue Shock syndrome): Aina hii ya homa ya dengue huambatana na mgonjwa kupoteza damu nyingi ambayo hupelekea mgonjwakupoteza fahamu. Dalili hizi zimeonekana kwa mgonjwa 1 kati ya wagonjwa 400 waliokwisha kuthibitishwa kuwa na ugonjwa hapa nchini.

## Matibabu

Homa ya dengue inaweza kutibika kama mgonjwa atapelekwa hospitali mapema na kupatiwa matibabu ya haraka.Hakuna dawa maalumu ya ugonjwa wala chanjo bali mgonjwa anatibiwa kutokana na dalili zitakazoambatana na ugonjwa huu kama vile homa, kupungukiwa maji au damu. Endapo mgonjwa atachelewa kupatiwa matibabu, mgonjwa anaweza kupoteza maisha.

## Jinsi ya Kujikinga

Jinsi ya kujikinga na ugonjwa wa homa ya dengue kuangamiza mazalio ya mbu, fukia madimbwi ya maji yaliyotuama au nyunyuzia viuatilifu vya kuua viluwiluwi vya mbu kwenye madimbwi hayo. Ondoa vitu vyote vinavyoweza kuweka mazalio ya mbu kama vile: vifuu vya nazi, makopo, magurudumu ya magari yaliyotupwa hovyo, nk. Fyeka vichaka vilivyo karibu na makazi ya watu. Hakikisha maua yanaayopandwa kwenye makopo au ndoo hayaruhusu maji kutuama. Funika mashimo ya maji taka kwa mfuniko imara. Safisha gata za paa la nyumba ili kutoruhusu maji kutuama. Kujikinga na kuumwa na mbu Tumia viuatilifu vya kufukuza mbu. Vaa nguo ndefu kujikinga na kuumwa na mbu. Tumia vyandarua vilivyosindikwa viuatilifu (kwa wale wanaolala majira ya mchana na hasa kwa watoto). Weka nyavu kwenye madirisha na milango ya nyumba za kuishi.

Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi, Muhimbili
S.L.P 65001, United Nations Road, Upanga West,
Dar es Salaam, TANZANIA
Simu: +255 22 2150473
Nukushi: +255 22 2150465
Anuani pepe: dvcarc@muhas.ac.tz
Tovuti: www.muhas.ac.tz